**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

SHULE YA SEKONDARI SINYA,
S.L.P.51,
**LONGIDO - ARUSHA**

EMAIL: andrewetekwi@gmail.com

Tarehe.............

Namba za simu.

**Mkuu wa shule: 0788688281/0764556479**

MZAZI WA ________________________________

S.L.P. ________MKOA________________________

PICHA P/S YA WAZAZI NA MTOTO

**MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SINYA ILIYOPO HALMASHAURI YA WILAYA YA LONGIDO MKOA WA ARUSHA MWAKA ....................... KIDATO CHA TANO.**

1.0. Nafurahi kukufahamisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha tano(V) katika shule hii mwaka .............. kwa tahasusi ya

| **HGK** | **HGL** | **HKL** |
|---|---|---|

**MAHALI SHULE ILIPO**

Shule ya Sekondari ya SINYA ipo katika Mkoa wa Arusha, Wilaya ya Longido, Tarafa ya Enduimet, kata ya SINYA, kijiji cha Endonyomali umbali wa KM46 kutoka makao makuu ya wilaya.

**JINSI YA KUFIKA SHULENI**

Kwa Wanafunzi wanaopitia barabara ya ARUSHA-LONGIDO washukie **longido na kuchukua usafiri kuelekea Sinya kupitia barabara ya Longido -Siha na ukifika geti la WMA-Ngasurai utakuta barabara inayoelekea upande wa kushoto kama unatokea longido ndiyo barabara ya kufika Sinya sekondari**, Kwa watakaopitia Moshi wapande magari yaendayo Arusha washukie **Boma Ng'ombe** wapande magari ya Kwenda **SANYA JUU** ambapo hapo watashuka na kupanda magari yaliyoandaliwa kwenda Sinya kwa siku hiyo ya kwanza ya kuripoti shuleni.

NB: Tarehe ya kuripoti (Zingatia tarehe iliyotangazwa na TAMISEMI kuhusu tarehe ya kuripoti shuleni)

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1. SARE YA SHULE WASICHANA.**

a) Sare ya shule ni

1 Sketi rangi NYEUSI iliyokolea mbili (02), urefu juu kidogo ya unyayo na isiyobana mwili, mshono rinda box (Kwa maulizo 0788688281.
Hatupokei kabisa sketi fupi.
2. Mashati meupe mikono mirefu mawili (02)
3. Tai ya rangi NYEUSI mbili (02)
4. Sweta RANGI NYEUSI moja (01) yenye shingo ‘V’.
5. Soksi nyeupe jozi mbili (02) (Stockings)
6. T-shirt Moja (01) (Mtindo wa Form Six) inapatikana shuleni ikiwa na Nembo ya shule.
7. Nguo ya kushindia (Shamba dress) rangi ya BLUE BAHARI mtindo wa solo.
8 Hijab (kijuba) nyeupe inayoishia chini ya kifua (kwa waislamu)
9 Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye kisigino kifupi.
10. Sare ya michezo ni Bukta na T- shirt (jezi) pair 01 rangi ya MARUNI (DAMU YA MZEE), Raba na Soksi.
11. Track suit rangi ya MARUNI (DAMU YA MZEE), yenye Nembo ya shule itapatikana shuleni.

**ZINGATIA**: Katika kukamilisha sare ya shule, nywele lazima ziwe fupi za kuchana, kucha ziwe fupi na zisipakwe rangi na uvaaji wa mapambo yoyote HAUTAKIWI.

**2.2. SARE ZA SHULE (WAVULANA)**

**(a)** Sare ya shule ni

1. Suruali rangi NYEUSI iliyokolea mbili (02) na isiyobana mwili (yenye marinda, yenye mkunjo wa chini na uwe na upana wa 17cm kwa chini) (Kwa maulizo 0788688281.Mashati meupe mikono mirefu mawili (02)
2. Tai ya rangi NYEUSI mbili (02)
3. Sweta RANGI NYEUSI moja (01) yenye shingo ‘V’.
4. Soksi nyeusi jozi mbili (02)
5. T-shirt Moja (01) (Mtindo wa Form Six) inapatikana shuleni ikiwa na Nembo ya shule.
6. Nguo ya kushindia (Shamba dress) suruali rangi ya BLUE BAHARI
7. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye kisigino kifupi.

8. Sare ya michezo ni Bukta na T- shirt (jezi) pair 01 rangi ya MARUNI (DAMU YA MZEE), Raba na Soksi.
9. Track suit rangi ya MARUNI (DAMU YA MZEE), yenye Nembo ya shule itapatikana shuleni.

**2.2 MICHANGO YA SHULE.**
**MICHANGO ANAYOTAKIWA KULIPA MZAZI.**

i. Nembo shilingi 5,000/=
ii. Kitambulisho cha shule Shilingi 5,000/=
iii. Tahadhari shilingi 5,000/=
iv. Uendeshaji wa shule Shilingi 65,000/=

**Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunt ya shule namba. 42510048024 Benki ya NMB Jina la Account ni Sinya Secondary School. (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye "pay in slip").**

**c) MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI NI:**

**i.** i **Rimu mbili (02) aina ya NO. 1 Photocopy paper size A4.**
**ii.** **Folder File ya kaki moja**, tafadhali usilete box file.
**iii.** Madaftari 12 kwa ajili ya masomo yake, Mathematical set, Graf pad, Kalamu na vifaa vingine vya kujifunzia.
**iv.** Begi la mgongoni la kuhifadhia vifaa vya darasani.
**v.** Squeezer 1 na soft broom 1

## 3.0MAHITAJI YA MALAZI YA BWENI.

i. Godoro (original) lenye ujazo wa sahihi na lenye upana wa futi mbili na nusu kwa sita ($2^{1/2}$x6), lenye foronya ngumu
   NB: Zingatia vipimo vya godoro viendane na vitanda vya shule
ii. Chandarua ya rangi nyeupe (01)
iii. Shuka rangi ya pink kwa wasichana na blue bahari kwa wavulana
iv. Blanketi moja (1) na mto wa kulalia.
v. Nguo za kulalia.
vi. Sanduku imara la kuhifadhia mali yako. (**Tunapokea sanduku moja tu aina ya tranka).**

ViiTaulo moja na vitenge doti moja (kwa wasichana).

vii. Mahitaji yote ya bafu kwa mfano. sabuni, mafuta, dawa ya meno.

viii. Ndoo ndogo mbili (02) kwa ajili ya matumizi binafsi

ix. Tochi 1 ya solar

xii Vyombo vya chakula (sahani, kijiko, kikombe na bakuli vyote vya aluminium

**4.0 MUHIMU KWA WANAJUMUIYA WA SINYA SEKONDARI.**

4.1 Wanafunzi wote lazima wafuate sheria za NCHI na za shule kwa ujumla. Lengo la sheria za shule yetu ni kumjenga mwanafunzi kuwa na mwenendo mzuri kitabia hivyo kumwezesha kufanikiwa kupata kile anachostahili haswa **Taaluma.**

Sheria hizi zitasaidia kuleta hali ya AMANI, UMOJA na FURAHA shuleni na kumfanya kuwa raia mwema. Kila mwanafunzi aje na nia ya KUSOMA KWA BIDII, KUJITUMA na ajitahidi kuishi vizuri katika jumuiya ya shule hii na majirani zetu pia

**4.2** Kwa upande wa shule sisi WALIMU pamoja na WAFANYAKAZI WASIO WALIMU tutajitahidi kumfundisha na kumlea mtoto katika maadili mema lakini tutashindwa kazi hii endapo hatutapata ushirikiano mzuri wa wazazi/walezi.Tunaomba ushirikiano wenu.

Kila mtu anatakiwa Kuheshimu:

**i.** **Bendera ya Taifa** na **picha za viongozi wa serikali**

ii. **Nembo ya Taifa “coat of Arms”, wimbo wa Taifa na fedha za Taifa**

Lugha inayotumika darasani na nje ya darasa ni Kiingereza tu. Hii inasaidia kuleta ufanisi katika masomo. Kwa vile shule ni mahali pa kusoma **kelele hazitakiwi kabisa** madarasani na sehemu nyingine za kujifunzia.

**4.3** Kila mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi vyote vinavyompasa kama Ratiba ya Shule inavyooelekeza. Kazi za mikono ni sehemu ya elimu inayotolewa hapa shuleni. Kila mmoja lazima ashiriki kikamilifu kazi za mikono.

**5.0 SHERIA ZA SHULE**

i Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotelewa na wizara ya Elimu na mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanya kazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na ya nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (prepation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
i) Kutunza mali za umma.

**6.0**. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga.
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g) Kudharau bendera ya Taifa.
h) Kuwa mjamzito/ kupata mimba
i) Kuoa au kuolewa
j) Kutoa mimba
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
m) Kuwa na simu ya mkononi.

**7.0 VIAMBATANISHO MUHIMU.**

a) Fomu ya utii na tabia njema kwa mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo,fujo,makosa ya jinai n.k
b) Fomu ya mzazi/mlezi historia na kukiri kukubaliana na sheria,kanuni za shule na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
c) Fomu ya uchunguzi wa afya (Medical Examination form) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa Hospitali ya Serikali.**Tafadhali ambatanisha majibu ya vipimo**.
d) Passport size ya Mwanafunzi, Baba, Mama au Walezi wake. **ZINGATIA:Tafadhali jaza fomu zote kwa ukamilifu**

**8.0. FOMU YA UTII NA TABIA NJEMA**

Mimi ------------------------------------------------------------------ (jina kamili la mwanafunzi)
Kidato cha -------------------------- mwaka ------------------
Natambua wajibu wangu kwa Taifa kama mwanafunzi na naahidi kwamba: -

a) Nitatii na kuwaheshimu viongozi wangu wote kuanzia ngazi ya darasa, viranja, walimu, watumishi wote hadi Mkuu wa Shule.

b) Nitafuata sheria na kanuni zote za shule pamoja na maelekezo yote yanayotolewa mara kwa mara na uongozi wa shule.

c) Sitashiriki katika mgomo,Fujo na makosa ya jinai.

d) Sitatoka nje ya mipaka ya shule wakati wa masomo labda tu kwa shughuli maalumu na baada ya kupata kibali maalumu kutoka kwa Mwalimu au Mkuu wa Shule mwenyewe.

e) Kama nitashindwa kufuata hayo yote hapo juu, hatua kali ichukuliwe dhidi yangu ni pamoja na kusimamishwa masomo ama kufukuzwa shule.

Tarehe --------------------- Jina na Sahihi ya Mwanafunzi------------------------------------------
Tarehe----------------------Jina la Mzazi/Mlezi-------------------------------------------------------

Sahihi ya Mkuu wa Shule-------------------------------------------

**9.0. FOMU YA TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI**

1. Jina kamili la Baba ----------------------------------------------------------------------
   Kazi yako-----------------------------------------------------------------------------
   Anwani ya mahali pa kazi ya baba ------------------------------------------------------
   Nambari ya simu ---------------------------------------------------------------------
2. Jina kamili la Mama --------------------------------------------------------------------
   Kazi yake ---------------------------------------------------------------------------
   Anwani ya mahali pa kazi ya mama ----------------------------------------------------
   Nambari ya simu ---------------------------------------------------------------------
3. Jina kamili la Mlezi (iwapo mtoto ni yatima)
   ___________________________________________
   Kazi na Anwani yaMzazi/ Mlezi -------------------------------------------------------
4. Nyumbani kwa baba (alipozaliwa mtoto) au 'Place of Domicile'
   Kijiji/Mtaa ------------------------------------ Wilaya ---------------------------------------
   Kata --------------------------------------------- Mkoa -----------------------------------------
   Tarafa -------------------------------------------
5. Mtoto anaishi na (i) Baba tu [ ] (ii) Mama tu [ ] (iii) Wazazi wote [ ] (iv) Walezi [ ]
6. Dini ya Baba ------------------------------------------ Dhehebu -------------------------
   Dini ya Mama ---------------------------------------- Dhehebu --------------------------
   Dhehebu unalotaka mwanao alelewe --------------------------------------------------

Nimesoma na kuelewa sheria na kanuni za shule.Nakubali kulipa michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.Nathibitisha kuwa taarifa hiyo hapo juu ni sahihi na naahidi kushirikiana na walimu ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo.Endapo mtoto wangu atashindwa kufuata hayo yote hatua kali dhidi yake zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kusimamishwa masomo au kufukuzwa shule.

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

Tarehe -----------------------------------------------
Jina la Mzazi/Mlezi----------------------------------------------------
Sahihi ya Mzazi/Mlezi ---------------------------------------
**MHIMU SANA**: Hakikisha umemkatia bima ya afya mwanao au aje na Tsh 6000 kwa ajili ya bima ya CHF.

10.0 **VITABU**

Ifuatayo ni baadhi ya orodha ya vitabu vinavyotumika darasani.

**GEOGRAPHY:**

1. Landforms in Africa by COLIN BUCKLE.
2. Principles of Physical Geography by MONKHOUSE.
3. Geography. Integrated Approach by WAUGH.
4. Practical Geography for Africa by J.M. PRITCHARD.
5. AFRICA by J.M. PRITCHARD.
6. Tropical Lands by MICHAEL SENIOR.
7. Human and Economic geography by MORGAN.
8. Comprehensive approach to physical geography by D.T. MSABILA
9. Elemantary physical geography by A. LUBWAMA
10. Practical geography for high schools and colleges by ZIST KAMILI
11. The essentials of practical geography a level form 5 & 6 by JOSEPH WILLIAM NJIKU & SALASU JACOB
12. Regional and human geography D.T. MSABILA

**HISTORY:**

1. Understanding African history paper one by JOHANES BIGRWAMUNGU
2. Understanding world history paper two JOHANES BIGRWAMUNGU
3. Essentials in advanced level history paper one SALEHE YASSIN
4. Essentials in advanced level history paper two SALEHE YASSIN
5. Contemporary historical events - history one COMRADE SHIBITALI C.K TUMAINI
6. Contemporary historical events - history two COMRADE SHIBITALI C.K TUMAINI
7. Major evets in the world history – history two GERVAS M. ZOMBWE
8. Lesson notes for advance certificate of secondary education - history one MWL. BAKARI MADAYA

**KISWAHILI:**

1. Tahakiki nyambari nyangwine kufikirika SHABANI ROBER
2. Vuta ni kuvute shafi by ADAM SHAFI
3. Usiku utakapo kwisha by MBUNDA MSOKILE
4. Uhungu tamu by T.A MVUNGI
5. Fungate ya uhuru by MOHAMED S. KHATIBU
6. Mapenzi bora by MKUKI NA NYOTA
7. Tahakiki by J MASEBO

ENGLISH LANGUAGE

1. Nyambari Nyangwine(2015) Advanced English language form 5 and 6, Nyambari Publishers, Dar-essalaam

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

SINYA SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX.51,
LONGIDO
Date. ------------------

Ref.SSS/F.V 2026/2027

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**PART A:**

Ref. No:

Medical Officer Date: ------------------------

-------------------------------------------

-------------------------------------------

-------------------------------------------

STUDENT'S NAME_______________________________________________

COMBINATION_________________________________________________

Please examine the named above for fitness for admission as a student of this school.

**PLEASE BRING TO SCHOOL THE DIAGNOSIS FORM**

Thank you.

**PART B:**

MEDICAL CERTIFICATE

(*To be completed by a Medical Officer*)

I have examined the above-named student and consider that she is fit/not fit for studies:

Explanation if any ------------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------

Date -------------------------------------------------- Signature ---------------------------------